

SHULE YA SEKONDARI KILEO DAY

S.L.P 304

BARUA PEPE [ezekieljossam@gmail.com](mailto:ezekieljossam@gmail.com)

SIMU 0672311831

TAREHE .....

Kumb Na .....

Jina la Mwanafunzi .....

S.L.P .....

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KILEO DAY,**

**WILAYA YA MWANGA MKOA WA KILIMANJARO MWAKA 2021**

1. UTANGULIZI.

Ninafuraha kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga kidato cha Kwanza katika shule hii **mwaka 2021**. Muhula wa kwanza wa masomo unaanza tarehe **11-01-2021** unatakiwa kuripoti shulenii kuanzia tarehe **11-01-2021** na mwisho wa kuripoti ni tarehe **18-01-2021** ndani ya siku saba.

2. SARE YA SHULE.

- Suruali ya heshima** (rangi imeambatanishwa) na shati jeupe la mikono mifupi, viatu vyeusi nya kufunga kamba kwa wavulana na **Sketi ndefu ya heshima** (rangi imeambatanishwa) na shati nyeupe mikono mifupi, viatu nya kufunga na kamba na vyenye visigino vifupi, na soksi nyeupe kwa wasichana.
- Rangi ya Hijabu nyeupe kwa wanafunzi wasichana wa kiislamu.
- Sare za michezo kwa shule hii ni bukta na tisheti ya blue pamoja na raba za michezo.

### 3. VIFAA VYA DARASANI.

Mzazi mnunulie mwanao madaftari ya kutosha, kalamu za wino na kalamu za risasi, mkebe wa hesabu, kamusi na dictionary.

### 4. CHAKULA CHA WANAFUNZI WA KUTWA.

Kikao cha wazazi kimekaa na kukubaliana chakula cha wanafunzi wa kutwa kwa mwaka ni **Tsh 87,000/=**, kwa muhula ni **Tsh 43,500/=**. Fedha hizo ziwekwe CRDB Bank A/C 015C438362200 Jina la Akaunti ni **KILEO SEKONDARI CHAKULA**.

### 5. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII.

Shule inaendeshwa kwa mujimu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1987 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na mafunzo ya Ufundu, yenyenye dhamana ya elimu nchini na Ofisi ya Raisi – TAMISEMI yenyenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo:-

- a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
- b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani nan je ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
- c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation)
- d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
- e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
- f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
- g) Kuvaal sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
- h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
- i) Kutunza mali za umma.

**6. MAKOSA YAFUATAYO YANAYOWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA SHULE AU  
KUSIMAMISHWA SHULE**

- a) Wizi.
- b) Uasherati na ushoga.
- c) Ubakaji.
- d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji wa bangi, cocaine, mirungi, kubeli na kadhalika.
- e) Kupigana au kupiga.
- f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
- g) Kudharau Bendera ya Taifa.
- h) Kuwa mjamzito/kupata mimba.
- i) Kuoa au kuolewa.
- j) Kutoa mimba.
- k) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
- l) Kukataa adhabu kwa makusudi.
- m) Kuwa na simu ya mkononi.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

